ST. `THOMAS HIGH SCHOOL

P.O. Box 40015, TEL: MOB: 0757-700401 / 0652-150403 / 0742-526304
GONGOLAMBOTO - DAR ES SALAAM.
www.thomasschools.ac.tz

SHULE IMESAJILIWA NA WIZARA YA LIMU KWA No. S.1343 NA NI KITUO CHA MITIHANI YA TAIFA (NECTA) No. S.1388

FOMU YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA:……

Gharama ya fomu ni Sh. 10,000/=

PICHA PASSPORT SIZE

FOMU NAMBA: ……..

JINA KAMILI LA MWANAFUNZI:	
TAREHE NA MWAKA WA KUZALIWA:	
URAIA:	
DINI:	
MAHALI ANAPOISHI:	
JINA LA SHULE YA MSINGI ULIYOSOMA:	
NAMBA YAKO YA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE:	
JINA LA SHULE YA SEKONDARI ULIYOTOKA:	
MWAKA ULIYOFANYA MTIHANI KIDATO CHA NNE:	
JINA LA MZAZI au MLEZI:	
NAMBA YA SIMU YA MZAZI au MLEZI:	
KAZI YA MZAZI au MLEZI:	
JINA LA NDUGU WA KARIBU:	
NAMBA YA SIMU YA NDUGU WA KARIBU:	

Shule ya Sekondari Thomas ina madarasa ya kidato cha Tano kwa masomo ya Sanaa (Arts) Biashara na Sayansi kama ifuatavyo:

1)	History, Geography na Kiingereza	-	(HGL)
2)	Economics, Geography na Mathematics	-	(EGM)
3)	History, Geography na Kiswahili	-	(HGK)
4)	History, Geography na Economics	-	(HGE)
5)	History, Kiswahili na English	-	(HKL)
6)	Chemistry, Biology na Geography	-	(CBG)
7)	Physics, Chemistry na Mathematics	-	(PCM)
8)	Physics, Chemistry na Biology	-	(PCB)
9)	Economics, Commerce, Accountancy	-	(ECA)

Somo la Computer litafundishwa bure kwa wanafunzi wote.

SIFA ZA MWOMBAJI ANAYETAKA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO

Mwanafunzi atakayejiunga na masomo hayo ni lazima awe amemaliza kidato cha nne (IV) amefaulu kwa kuwa na alama **C** katika masomo matatu (Yaani awe na alama C zisizopungua 3), kwa masomo yoyote isipokuwa ya dini. Na kwa wale ambao wana **C 1** au **C 2** watajiunga na kidato cha **V** lakini watareseat kwa ajili ya kupata Credit za kumuwezesha kufanya mtihani wa kidato cha sita kwa hivyo kama atataka kufanya mtihani wa kidato cha sita kama mtahiniwa wa shule atasoma kwa muda wa miaka mitatu (3) na kama atataka kufanya mtihani kama mtahiniwa wa kujitegemea atasoma miaka miwili (2) Masomo yataanza rasmi tarehe: ……

<u>TAARIFA ZA KIAFYA ZA MWANAFUNZI:</u>

Mzazi/Mlezi Unatakiwa Kutoa Maelezo ya ukweli Kuhusu Afya Ya Mwanafunzi Maelezo hayo Yaambatanishwe Na Uthibitisho Wa Daktari Kama Mwanafunzi Ana Matatizo Ya Kiafya:…….

……

……

……..

GHARAMA ZA ADA YA MASOMO, NA MICHANGO NI KAMA IFUATAVYO:

A:

MUHULA	**ADA**
AWAMU YA KWANZA: JULAI - DISEMBA	**500,000**
AWAMU YA PILI: JANUARY - APRIL	**200,000**
KITAMBULISHO	**10,000**
SARE PEA MBILI NA T-SHIRT MOJA	**81,000**
JUMLA	**791,000**

B:

HOSTEL	**T.SH.**
AWAMU YA KWANZA: JULAI - DISEMBA	**450,000**
AWAMU YA PILI: JANUARI - APRIL	**450,000**
JUMLA	**900,000**

ADA ILIPWE CRDB BANK KUPITIA AKAUNTI NA MICHANGO YOTE ILIPWE OFISI YA MUHASIBU

JINA LA AKAUNTI - CRDB BANK	**NAMBARI YA AKAUNTI**

`Kwa wale ambao wana upungufu wa credit watasoma masomo ya kurudia kwa gharama ya Tshs. **250,000/=** kwa mwaka watalipa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza Tsh. **125,000/=** na awamu ya pili ni Tshs. **125,000/=.** Mzazi utalazimika kulipa gharama za mtihani wa kurudia na usajili Posta.

TAARIFA ZA SHULE:

1. Masomo yataanza rasmi tarehe **20 Julai 2020**
2. Ada ya shule ni Tsh. Laki saba tu kwa mwaka **(700,000/=)**
3. Ada italipwa kwa awamu nne kama ilivyoanishwa katika jedwali hapo juu, na malipo yote ya ada na michango yalipwe shuleni ofisi ya Mhasibu na utapewa stakabadhi ya shule kwa malipo uliyolipa.
4. Mwanafunzi anatakiwa kuja na rim mbili kila muhula za karatasi nyeupe za A4 size moja na zenye mistari rim moja.
5. Mwanafunzi aliyepata Division One atapewa ofa ya kulipia ada shillingi laki sita **(600,000/=)** kwa mwaka badala ya laki saba **(700,000/=)** kwa mwaka (kwa kidato cha tano tu)
6. Ada ya hosteli ni shilingi laki tisa **(900,000/=)** kwa mwaka na italipwa kwa awamu mbili.

TAHADHARI:

- **Tunakutahadharisha ndugu mzazi/mlezi hairuhusiwi kulipa au kutoa pesa za ada au michango kwa Mwalimu au kutuma pesa kupitia simu. Hakuna mwalimu yoyote anayehusika kupokea ada au malipo ya michango ya shule. Hakikisha unalipa ada Benki na michango utalipia shuleni ofisi ya muhasibu na unapewa stakabadhi kwa kila malipo unayolipa. Mwanafunzi hataruhusiwa kuanza masomo bila kukamilisha malipo ya ada na michango.**

SARE ZA SHULE KWA WAVULANA:

1. Suruali ya blue
2. Shati jeupe
3. T-shirt ya kijivu yenye kola (form six)
4. Soksi nyeusi
5. Viatu vyeusi vya ngozi.
6. Tai ya dark blue.
7. Nembo ya shule.

SARE ZA SHULE KWA WASICHANA:

1. Sketi ya blue
2. Shati jeupe
3. T- shirt ya kijivu (form six)
4. Soksi ndefu Nyeupe
5. Viatu vyeusi vya ngozi.
6. Tai ya dark blue.
7. Nembo ya shule.
8. Hijabu kwa atakayependa (iwe ndefu).

- Uvaaji wa HIJABU unaruhusiwa kwa waislamu tu, vinginevyo ni kinyume na taratibu

NB: Sare za shule zitashoneshwa shuleni gharama **zilipwe kabla ya kuanza masomo** kwa sketi mbili / suruali mbili,mashati mawili, nembo, tai, T shirt.

SHERIA ZA SHULE:

1. Sare za shule HAZITAKIWI kubana maumbile.
2. Soksi za shule HAZITAKIWI kuwa fupi.
3. Viatu vya shule ni lazima kuwa vya ngozi.
4. Kwa wasichana HAWARUHUSIWI kusuka zaidi au pungufu ya nywele tano tu na hairuhusiwi kuweka nywele dawa. Kwa wavulana HAIRUHUSIWI kufuga ndevu na kunyoa nywele kwa ukubwa tofauti; upara au kuweka alama yoyote kichwani.
5. HAIRUHUSIWI kufuga kucha wala kupaka kucha rangi au kuchora mwili.

6. Sketi inatakiwa kuwa ndefu kuzidi magoti
7. Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, cheni, bangili au urembo wa aina yoyote.
8. Hairuhusiwi kupaka vipodozi vya aina yoyote.
9. Hairuhusiwi kula chakula darasani.

MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

1. Kukamatwa na simu ya mkononi
2. Kutumia lugha chafu au matusi
3. Kupigana au ugomvi
4. Wizi, utapeli
5. Uzinifu iwe ni nje au ndani ya shule (Uasherati)
6. Utoro, na uzembe wa makusudi katika masomo.
7. Matumizi ya dawa za kulevya, ulevi, kunywa pombe kuvuta bangi au sigara.
8. Kugomea adhabu utakazopewa na walimu
9. Utovu wa nidhamu wa aina yoyote.

Kila Mwanafunzi anatakiwa kufuata sheria zote za shule kama zilivyoainishwa katika kipengele cha sheria za shule.

NGUO KWA MWANAFUNZI WA HOSTEL

- Vest rangi nyeupe zisiwe chini ya nne (4) nunua popote.
- Suruali ya truck suit rangi bluu itatumika siku ya michezo na wakati wa kujisomea nyakati za usiku.
- T-shirt rangi nyeupe isiyo na maandishi idadi yoyote
- Raba nyeupe za kufunga kamba.
- Viatu vya michezo.

VIFAA ANAVYOPASWA KUJA NAVYO MWANAFUNZI:

1) Chandarua itanayotosha kufunika kitanda cha futi 3½ kwa futi 6
2) Shuka pea mbili za kutosha kutandika kitanda cha futi 3½ kwa futi 6. Pea moja iwe nyeupe kwa ajili ya siku ya ukaguzi.
3) Godoro la futi 2½ au futi 3, inch 2½
4) Vyombo vya kulia chakula, Sahani, kijiko, kikombe kikubwa mfano wa Mug na visiwe vya plastic.
5) Ndoo ndogo na kopo kwa ajili ya kuogea na kufulia.
6) Vifaa vya kutosha vya kutumia mwanafunzi awapo Hostel mfano Sabuni za kuogea na kufulia, pamba, nyembe, kalamu, madaftari n.k.

SIFA ANAZOTAKIWA KUWA NAZO MWOMBAJI WA KUJIUNGA NI:

1) Awe na nidhamu ya hali ya juu.
2) Awe na afya njema (asiwe na matatizo ya kiafya, asiyehitaji chakula maalumu (Special diet)
3) Awe tayari kuonyesha ushirikiano wa kuzitii sheria za Hostel
4) Kutovunja sheria nyingine zozote za nchi na wizara.

SHERIA ZA HOSTEL

1) Hairuhusiwi kuvuka mipaka au kutoka nje ya Hosteli bila ruhusa kutoka kwa Mkuu wa Shule.
2) Hairuhusiwi kupika wala kuingiza chakula chochote kutoka nje ya Hosteli
3) Hairuhusiwi kuingiza wala kunywa pombe na kuvuta sigara hosteli
4) Hairuhusiwi kulala watu wawili kitanda kimoja.

5) Hairuhusiwi kubandika picha wala kuandika katika kuta za majengo ya Hostel
6) Hairuhusiwi kutoa mimba, uzinzi, uongo, matusi na wizi.
7) Hairuhusiwi kuingiza mtu asiye mwanahosteli vyumbani.
8) Kila mwanahostel atatakiwa kushiriki kazi zote za hosteli, ikiwa ni sehemu ya somo la kujitegemea.
9) Kila mwanahostel atatakiwa kuvaa sare ya Hostel wakati wote isipokuwa siku zilizoamriwa.
10) Hairuhusiwi kuwa na simu za mkononi.
11) Ni lazima kila mwanafunzi ahudhurie prepo kuanzia saa **2:00** usiku hadi saa **4:00** usiku.
12) Ni lazima mwanafunzi afanye mazoezi kila siku asubuhi saa **11:00** alfajiri hadi saa **12:00** asubuhi.

WAGENI WANAOWEZA KUMTEMBELEA MWANAHOSTEL:

1. …… Uhusiano: ……..
2. …… Uhusiano: ……..
3. …… Uhusiano: ……..

NB: Mabadiliko katika sheria na malipo yanaweza kubadilika wakati wowote utafahamishwa kama itatokea.

Sahihi:…….. Tarehe: ……

FOMU HII ITARUDISHWA OFISINI KWA MSAJILI WA WANAFUNZI IKIAMBATANISHWA NA PICHA 2 PASSPORT SIZE PAMOJA NA NAKALA YA CHETI CHA MATOKEO YA KIDATO CHA NNE AU RESULTS SLIP.

****Kumbuka elimu ndio urithi pekee na wa kudumu, Elimu ni Silaha ya umasikini****

MKUU WA SHULE

THOMAS HIGH SCHOOL